

## SKPS itapunguza idadi ya wanafunzi wanaosaidiwa kwa kwenda shule na itasimamisha shughuli zote za michezo

Siku ya Ijumaa tarehe 13 Novemba Gavana wa Oregon Kate Brown alitangaza kusimamisha shughuli zenye mikusanyiko ya watu katika kipindi cha wiki mbili ambazo zitaanza Jumatano tarehe 18 Novemba. Baada ya kupokea mwongozo wa ziada kutoka Idara ya elimu ya Oregon, tumefanya uamuzi mgumu kupunguza namba ya wafunzi ambao huenda mashuleni kwa msaada zaidi na kusimamaisha shughuli zote za michezo katika shule zote.

Mambo muhimu ya kujua:

- Kuanzia Jumatatu tarehe 16 Novemba, mazoezi yote ya ziada na shughuli zote za michezo zimesitishwa.
- Ikiwa shule yako inampango wa kugawa vitu au kusambaza au kufundisha watu wachache shuleni inaweza kuendelea mpaka Jumatano. Shule yako itawasiliana na wewe moja kwa moja juu mipango hiyo.
- Chakula kitaendelea kugawia Jumatatu hadi Ijumaa kutoka saa 5 asubuhi mpaka saa 7 mchana (11am-1pm) Orodha ya shule zinazogawa chakula zinapatikana kwenye tovuti ya shule za Wilaya ya Salem-Keizer.
- Ofisi za shule zitafungwa kwa umma, lakini unaweza kuwasiliana na shule kwa njia ya simu Jumatatu – Ijumaa.

Maamuzi haya hayakuwa rahisi kwani tunatambua ya kuwa baadhi ya wanafunzi wale wanaohitaji msaada wa zaidi waliweza kusaidiwa katika hiki kipindi cha masomo ya kwenye mtandao. Tutaendelea kujitahidi kuwasaidia wanafunzi katika masomo.

Tunaungana na jumuiya yetu katika kupunguza kasi ya kusambaa na kueneza maambukizi ya Covid 19. Tunajitahidi kufanya kila kitu ili kulinda na kuwasaidia familia ya SKPS na jumuiya ya Salem – Keizer.